# Kamati ya Bunge yaipongeza TEA utekelezaji miradi ya elimu Zanzibar

NA MWANDISHI WETU, ZANZIBAR

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imesema kwa miaka mitano iliyopita imetumia bilioni 2.8 kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu nchini ikiwemo kuwapa mafunzo ya kuendeleza ujuzi vijana 600 kutoka kaya maskini.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Erasmus Kipesha, wakati akizungumza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, iliyotembelea miradi ya mamlaka hiyo visiwani Zanzibar.

Ziara hiyo ililenga kukagua na kutathmini maendeleo ya miradi ya elimu inayotekelezwa na TEA pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za muungano katika sekta ya elimu.

Alisema kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2.1 zimetumika kuboresha miundombinu ya elimu, huku shilingi milioni 574.3 zikielekezwa katika kufadhili Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi (SDF) kwa vijana kutoka kaya maskini.

"Kwa kipindi hicho tumejenga madarasa, vyoo vya shule, kukarabati shule nyingi mkongwe na kujenga nyumba za walimu kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni jitihada za kuboresha mazingira ya kusomea ili kuinua kiwango cha elimu," alisema

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Dk Leonard Akwilapo, aliishukuru Kamati ya Bunge kwa kutambua juhudi za Mamlaka hiyo na kuahidi kuendelea kusimamia kwa weledi utekelezaji wa miradi yote ya elimu Tanzania Bara na Zanzibar.

Pia alisisitiza kuwa TEA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutafuta rasilimali kifedha ili kufadhili miradi mingi zaidi kwa maendeleo ya sekta ya elimu hapa nchini.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Florent Kyombo, alipongeza (TEA) kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake, hususani miradi ya elimu inayotekelezwa Zanzibar.

Alisema mamlaka hiyo imefanya juhudi kubwa kuboresha miundombinu ya elimu na kuongeza fursa za ujifunzaji na ufundishaji katika ngazi zote za elimu.

Kyombo alisisitiza kuwa TEA imefanya kazi kubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu, na miradi yake imekuwa na manufaa makubwa kwa jamii.

Alibainisha kuwa hata jimboni kwake, TEA imetekeleza miradi kadhaa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, hali inayosaidia wanafunzi kusoma kwenye mazingira mzuri hivyo kuinua kiwango cha taaluma nchini.

"TEA imefanya kazi kubwa sana kwenye uboreshaji wa miundombinu ya elimu kote nchini, siyo Zanzibar pekee. Ukipita maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji, utaiona miradi yao mingi ambayo inaendelea kutatua changamoto za miundombinu ya elimu," alisema Kyombo.

Aidha, alishauri TEA kupanua wigo wa utekelezaji wa miradi ya uendelezaji ujuzi ili kutoa fursa kwa watanzania wengi zaidi kunufaika, hasa katika kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Miongoni mwa majukumu ya TEA ni kutafuta raslimali fedha kutoka kwa wadau mbali mbali na kuzitumia kujenga miundombinu ya elimu katika taasisi za elimu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia .

# Tume ya haki za binadamu kukutana na makundi mbalimbali mkoani Iringa

NA BERDINA MAJINGE
MATUKIO DAIMA MEDIA ,
IRINGA

TUME ya haki za binadamu na utawala bora nchini imesema kuwa inatarajia kutoa elimu katika maeneo ambayo wananchi wanazuiliwa kufika ili kuwasaidia watu walioko katika mazingira hayo kujua haki zao za msingi.

Elimu hiyo itatolewa katika magereza, kituo cha Polisi cha kati wakiangalia viwango vya uzingatiaji wa haki za binadamu katika maeneo hayo na ufuatiliaji wake.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Iringa, Kamishina wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora Dkt Thomas Masanja alisema kuwa wanatarajia kutoa elimu hiyo maeneo mbalimbali katika mkoa huo kwa siku 20.

Dkt Masanja alisema kuwa elimu hiyo itatolewa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, wanafunzi wa shule za sekondari, watendaji wa mitaa na vijiji, magereza na kituo cha polisi cha kati mkoani Iringa.

"Tuko Mkoani hapa kuendeleza haki za binadamu na utawala bora ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na kufanya tafiti mbalimbali juu ya masuala ya haki za binadamu na kuishauri serikali juu ya masuala yanayokiukwa kwa wananchi"

Alisema kuwa tume inaangalia na kuwafikia watu wenye ulemavu wa ngozi kwa kufanya mikutano ya hadhara kupitia watendaji wavijiji.

"Mwananchi anapokuwa gerezani anakuwa amenyang'anywa uhuru lakini haki zake zingine zote anabaki nazo ikiongozwa na haki ya utu wa mtu ambayo kila mtu anazaliwa nayo, pia haki zingine ni kupata matibabu pamoja na chakula"

Dkt Masanja alieleza kuwa kupitia watendaji wa vijiji na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na shule za sekondali watafanikiwa kuwafikia wananchi wengi kupata elimu ya haki za binadamu na utawala bora.

Akizungumzia suala la wananchi kukamatwa siku ambazo si kazi na kunyimwa dhamana siku hizo Dkt Masanja alisema kuwa sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ni mtu atakamatwa na kuwekwa kizuizini mpaka pale upelelezi utakapo kuwa umekamilika lakini makosa mengine yanaelekeza baada ya uchunguzi na kujiridhisha kuwa hana hatia mtuhumiwa ataachiwa au kupewa dhamana.

Dkt Masanja alisema kuwa suala la wananchi kupotea au kuwa katika mazingira ambayo hayajulikani alisema kuwa tayari tume imetoa tamko na kusema kuwa wangefanya ufatiliaji kwa watu wanaodaiwa kupotea na walifanyakazi hiyo November 2024.



*Mwenyekiti wa Chama Cha waandishi wa habari mkoa wa Iringa (IPC) Frank Leonard akimkaribidha Kamishina wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora Dkt Thomas Masanja wa pili kushoto kuzungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani)mkoa wa Iringa. Picha na Matukio Daima Media*